
# Upatikanaji wa Huduma za Afya kwa Wote


## *MUHTASARI*

*Ili kufikia shabaha ya upatikanaji wa huduma za afya kwa wote nchini Tanzania kunahitajika mbinu mbalimbali, ikiwa ni pamoja na kuhamasisha upatikanaji wa mapato ya ndani, uwekezaji wa kimkakati katika miundombinu ya afya, kuendeleza nguvu kazi, na kufanya maandalizi kuelekea kwenye utaratibu wa kuweka ulazima wa bima ya afya kwa wote. Ikiwa juhudi hizi zitazingatiwa na kutatua kwa bidii changamoto za rasilimali, Tanzania inaweza kupiga hatua kubwa katika kuhakikisha upatikanaji wa huduma bora za afya kwa watu wote.*


## Utangulizi

Mafanikio ya Dira ya Maendeleo ya Tanzania 2025, yanategemea uanzishwaji wa mpango wa Afya kwa Wote (UHC), mfumo utakaohakikisha upatikanaji wa huduma bora za afya ya msingi bila kupata kikwazo cha kutakiwa kulipia gharama za huduma za matibabu wakati wa kupata huduma. Tafiti zinaonyesha kuwa, mpango wa Afya kwa Wote, sio tu utawezesha kufanya maisha yawe yenye afya, bali pia utachangia uwepo wa nguvu kazi imara zaidi na hivyo kukuza uchumi wa taifa. Ili kutimiza dira hii, serikali ya Tanzania imepitisha Mkakati wa Taifa wa uwezeshaji fedha katika Huduma za Afya nchini (2015/25), unaolenga kuanzisha mfuko mmoja wa taifa wa bima ya afya.




*Kielelezo cha 1: Miundombinu ya Afya na Nguvukazi kati ya mwaka 2007 na 2023*

## Uwekezaji katika miundombinu na rasilimali watu ili kufikia mpango wa afya kwa wote


Kufikia upatikanaji wa huduma za afya ya msingi kunahitaji uwekezaji mkubwa katika miundombinu ya huduma za afya na maendeleo ya watoa huduma, ili kupunguza umbali mrefu wa kusafiri na vizuizi vya kufikia huduma.

Sera ya Afya ya mwaka 2007 inaelekeza hitaji la zahanati katika kila kijiji, vituo vya afya katika kila kata na hospitali katika kila wilaya. Tangu mwaka 2007, serikali ya Tanzania na washirika wake wa maendeleo wamefanya kazi ya kuimarisha miundombinu ya afya na nguvu kazi nchini.

Juhudi endelevu za ujenzi na ukarabati zimeongeza upatikanaji wa miundombinu ya afya kutoka asilimia 41 ya mahitaji mwaka 2007, hadi asilimia 53 kwa mwaka 2023. Sambamba na hilo, juhudi za mafunzo na utoji wa ajira zimeongeza upatikanaji wa watoa huduma wa afya kutoka asilimia 35 ya mahitaji mwaka 2006, hadi asilimia 50 mwaka 2023. Takwimu hizi zinaonesha mwelekeo mzuri wa upatikanaji wa huduma za afya ya msingi, japo kwa kasi ndogo.

## Idadi ndogo ya wanufaika ambao wamejiunga katika Bima ya Afya

Licha ya maendeleo haya, idadi ya wananchi ambao wamejiunga na mifuko ya bima ya afya ikiwemo NHIF, CHF iliyoboreshwa na mifuko binafsi bado hairidhishi. Hadi kufikia Septemba 2023, asilimia 15.3 tu ya wananchi wa Tanzania ndio wapo katika mfumo wa bima ya afya ya umma na binafsi[1]. Hali hii imeacha sehemu kubwa ya wananchi hasa wale wasiojiweza, masikini na wale walioko maeneo ya vijijini.




*Kielelezo cha 2: Utayari katika Huduma na Fahirisi Ndogo kati ya 2012 na 2020*

[1] *Maelezo ya Mheshimiwa Ummy Ally Mwalimu (MB), Waziri wa Afya, akiwasilisha Muswada wa Kutunga Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote wa Mwaka 2022 katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 01 Novemba 2023*

Sababu kuu ya uandikishaji mdogo wa bima ya afya ni kutoridhishwa na ubora wa huduma za afya za msingi. Ripoti ya Tathmini ya Upatikanaji na Utayari wa Huduma (SARA) inatilia mkazo mapungufu ya msingi katika rasilimali muhimu ndani ya vituo vya kutolea huduma za afya. SARA inatathmini upatikanaji wa huduma za msingi katika vituo vya kutolea huduma za afya kama vile nishati, maji, vyumba vya madaktari, usafi wa mazingira, vifaa vya mawasiliano, upatikanaji wa mawasiliano, na usafiri wakati wa dharura.

Kwa miaka mingi, wastani wa upatikanaji wa vifaa hivi muhimu umeongezeka kwa kiasi kikubwa, kutoka asilimia 27 kwa mwaka 2012 hadi asilimia 85 mwaka 2020. Hata hivyo, upatikanaji wa vifaa muhimu ikiwa ni pamoja na mizani, stethoscopes, na vipima joto, umepungua kidogo kutoka asilimia 70 mwaka 2012 hadi asilimia 65 kwa mwaka 2020. Uwezo katika uchunguzi, ambao ni kipengele muhimu cha huduma bora, umeonekana kuimarika, huku upatikanaji ukiongezeka kutoka asilimia 29 kwa mwaka 2012 hadi asilimia 72 kwa mwaka 2020. Vilevile, uchukuaji wa tahadhari za kudhibiti magonjwa ambukizi umeongezeka kutoka, asilimia 46 kwa mwaka 2012 hadi asilimia 70 kwa mwaka 2020. Upatikanaji wa dawa muhimu, kama ilivyoainishwa kwenye orodha ya Kitaifa ya Dawa Muhimu (2017), uliongezeka kutoka asilimia 41 kwa mwaka 2012 hadi asilimia 54 kwa mwaka 2020.

Takwimu hizi kwa pamoja zinasisitiza maboresho kwenye utayari wa huduma. Pia, kutatua mapungufu ya rasilimali ambayo yanaendelea kuathiri ubora wa huduma.

## Kufikia mpango wa afya kwa wote

Katika miaka 16 iliyopita, uwekezaji kwenye miundombinu ya huduma za afya na nguvu kazi umefanyika. Hata hivyo, ongezeko la kasi la idadi ya watu na mahitaji umeleta changamoto katika kuhakikisha upatikanaji wa huduma za afya ya msingi. Ingawa uwezo wa vituo vya kutolea huduma za afya kwa ujumla umeimarika, ubora wa viwango vya juu vya huduma haujafikiwa kikamilifu. Kwa muktadha huu, kuanzisha Bima ya afya ya lazima kwa wote nchini bila kuhakikisha upatikanaji wa kuridhisha wa huduma za msingi vituoni, kunaweza kusababisha wananchi kukosa hamasa ya kujiunga na bima hiyo. Hivyo, maeneo ambayo hayajafikia viwango hivi ni vizuri kujikita katika kuboresha upatikanaji wa huduma za afya ya msingi kwanza.

Ili kufikia mpango wa afya kwa wote katika siku zijazo, kuna hitaji la kuongeza uwekezaji katika mifumo ya afya. Matumizi ya jumla ya serikali katika afya kupitia mapato ya ndani yameongezeka kutoka asilimia 1.2 ya pato la taifa kwa mwaka 2014 hadi asilimia 1.6 ya pato la taifa kwa mwaka 2020. Hata hivyo matumizi bado yapo chini ya kiwango kinacholengwa cha asilimia 5 ya pato la taifa. Hii inaashiria kuwa asilimia 5 ya lengo la pato la taifa haiwezi kufikiwa bila kutenga sehemu ya mapato ya ndani ya serikali kulingana na pato la taifa. Uchambuzi wa Sikika (2022) unapendekeza sera mbadala ya fedha ambayo inaweza kusaidia kuongeza mapato ya serikali kutoka asilimia 16.3 ya pato la taifa kwa mwaka 2019/2020 hadi makadirio ya mapato ya asilimia 25 ya pato la taifa.

## Mapendekezo

- Kuongeza mapato ya serikali hadi kufikia asilimia 25 ya pato la taifa.
- Kuongeza matumizi ya serikali kwenye afya yanayotokana na mapato ya ndani hadi kufikia asilimia 5 ya pato la taifa.
- Kutenga rasilimali za ziada ili kuhakikisha kuwa mfumo wa afya unakidhi ubora wa viwango vya juu vya huduma za afya.
- Kuanzisha bima ya afya ya lazima kwa wananchi katika maeneo ambayo ubora wa viwango vya juu vya huduma za afya umefikiwa.

**Sikika inafanya kazi ya kuhimiza uboreshaji wa mifumo ya afya na usimamizi wa fedha kupitia uwajibikaji jamii na uraghibishi katika ngazi zote za serikali**

**Uchambuzi huu umefadhiliwa na Foundation for Civil Society**

FOUNDATION FOR CIVIL SOCIETY
Facilitating Partnerships for Development

Sikika

Barabara ya Haile Salassie,
Mtaa wa Mwaya, Masaki
Nyumba Na. 10,
S.L.P 12183, Dar es Salaam,Tanzania.
Simu: +255 222 26 580 15

Ujumbe mfupi: 0688 493 882
Nukushi: +255 22 26 680 15
Barua pepe: info@sikika.or.tz
Tovuti: www.sikika.or.tz
Twitter: @sikika1
Facebook: sikika1
Instagram: sikika1
Linkedin: sikika Tanzania

Nyumba Na. 340
Mtaa wa Kilimani
S.L.P 1970 Dodoma, Tanzania.
Simu: 0262321307
Nukushi: 0262321316